# LEARNING BY EAR

## "WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA"

## KIPINDI CHA KUMI: ”NDIO TUNAWEZA!”

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: KATRIN OGUNSADE**

**HEALTH EXPERT: DR. HEIDRUN HÜBNER**

## SCENE ONE: MASIKA SINGING A LULLABY TO A CRYING ZAWADI

**CHARACTERS:**

- ZAWADI (BABY, no actor)
- MASIKA (m, 40)
- YAKUBU (m, 41)
- NARRATOR

## SCENE TWO: MAMA DAVID'S HOUSE

**CHARACTERS:**

- DAVID(m, 14)
- MAMA DAVID (f, 43)
- BETTINA (f, 34)
- KAREMBO (f, 14)
- NARRATOR

## SCENE THREE: MORNING AT KAREMBO'S SCHOOL ASSEMBLY

**CHARACTERS:**

- HEADTEACHER(38, female),
- STUDENTS IN CLASS / AT SCHOOL (AROUND 14 YEARS OLD)

- NARRATOR

**SCENE FOUR:MASIKA,BETINA AND YAKUBU AT MASIKAS HOME LISTENING TO RADIO**

**CHARACTERS:**

- MASIKA (m, 40)
- YAKUBU (m, 41)
- BETTINA (f, 34)
- RADIO PRESENTER (28)
- DR. MUNGA (m, 45)
- KAREMBO (f, 14)
- NARRATOR

**INTRO/NARRATOR:**

Natumai hujambo msikilizaji na karibu kwa mara nyingine katika mchezo wa kuigiza **"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA"**. Wiki iliyopita tuliishia katikati ya hamaki na kufokeana kati ya mamake david na mamake karembo na watoto wao kupigwa na butwaa kwa kuwakuta katika patashika hiyo. Shuleni nako je, karembo atafanikiwa na chama chale cha kuhimiza watu kuhusu madhara ya mbu na kuepuka ugonjwa wa malaria? Kisa cha Leo ni **" NDIO TUNAWEZA!"**.

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: MASIKA SINGING A LULLABY TO A CRYING ZAWADI</u>**

**A-SFX: BABY CRYING LOUDLY**

**1. MASIKA: (SINGING LULLABY BUT ZAWADI DOESN'T STOP CRYING)**

Sasa wataka nini Zawadi? **(FRUSTRATED)** na mamako amecheleweshwa na nini?nilijua haikua wazo zuri kumtuma kwa mama david..sasa ni gumzo weeee...

**B-SFX: BABY STILL CRYING..**

**2. MASIKA:** Haya njoo totoo... njoo... usilie babangu.... mfalme wa afrika.... njoo nikubebe...

**(ZAWADI STOPS CRYING)**

**C-SFX: HARD KNOCKING ON DOOR**

**3. MASIKA:** **(ANGRY AT THE SUDDEN INTRUSION)** Fujo hiyo ni ya nini? Hapawezi kuwa na amani humu nyumbani? Ingia mlango uko wazi!!!

**D-SFX: DOOR OPENS WITH SOUND OF OLD HINGES**

**4. YAKUBU: (PANICKY VOICE)** Masika! Masika!tafadhali nisaidie!

**5. MASIKA:** Sssh! Taratibu yakubu usiseme kwa kelele utaniamshia huyu mtoto wangu... kumetokea nini?

**6. YAKUBU:** Ni binti yangu yule mdogo, ni mgonjwa mahututi... hali, halali, hivi amebaki kifefe tafadhali nisaidie...

**7. MASIKA:** Sasa nikusaidiaje? Mimi sio daktari... mpeleke hospitali, utaelezwa kinachomsumbua... lakini kama ni malaria basi hata wewe pia ulichangia .nilikueleza kutumia neti za kujikingia mbu dhidi ya malaria kwa kuvulia samaki ni makosa lakini hukuyatilia maanani maneno yangu... mimi nilipata funzo jamii yangu ilipougua malaria na nikairudisha neti nyumbani.

**8. YAKUBU:** Huna akiba ya dawa ili tumpe hivi sasa? Hata kama ni dawa za zawadi lete tumpe kwani binti yangu amemzidi zawadi wako kwa miaka miwili tu..bila shaka zitamfaa...

**9. MASIKA:** Ninazo lakini sidhani kama ni uamuzi mzuri kukupa dawa hizo, ni hatari kutumia dawa ambazo hukuidhinishwa na daktari.. kamuone daktari Munga wa wilaya ya Ribo atakupa ushauri

**10. YAKUBU:** Sawa, lakini zaidi ya hayo.. tafadhali nifae na senti kidogo.. najuwa mwenzangu una akiba kwani mradi wako haukupeleki vibaya.. nitakulipa hivi karibuni.

**11. MASIKA:** Hamna wasiwasi..ngoja nimlaze huyu mtoto

**E-SFX (HANDS OVER BANK NOTES/ NOTES SHUFFLING)**

**12. MASIKA:** Baada ya kumpeleka binti yako hospitali... tafadhali njoo

iwapo unataka nikupe kazi angalau ujipatie pesa kidogo... samaki wamekuwa wengi na najuwa wewe una uzoefu wa kazi za samaki... njoo nitakuajiri...

**13. NARRATOR:** wengi wetu tunapenda kutoa dawa kwa watu wengine bila idhini ya daktari... hii inaweza kuhatarisha afya zetu na hasa iwapo inahusu watoto... masika alitumia busara yake kumkatalia Yakubu na hata labda kumuepusha binti yake na maafa mengine.. usisahau kule kando bado kuna ugomvi kati ya mamake david na mamake karembo watoto wao wakishuhudia...

**<u>SCENE TWO: MAMA DAVID'S HOUSE</u>**

**14. MAMA DAVID: (EMBARASSED)** David mwanangu... shuleni munaendeleaje? Karembo hujambo mama? Wajisikiaje sasa?

**15. BETTINA: (STILL ANGRY)** Karembo,unafanya nini huku?.

**16. KAREMBO:** nilipitia kwa mamake david ilinichukue nyasi..

**17. BETTINA:** Nyasi?nyasi gani?na ni za kazi gani?

**18. DAVID: (SCARED)** sio nyasi za kawaida .. ni zile nyasi za mzumai...

**19. MAMA DAVID:** kwani ulimueleza karembo kuhusu nyasi hizo?

**20. DAVID:** Ndio mama, nilimueleza. Hii ni njia moja wapo ya kufukuza mbu amabyo ni salama kwa mazingira yetu... nilifikiri ni muhimu kueleza kijiji chote kuhusu nyasi hizo...

**21. BETTINA:** Hebu nielezeni kinachoendelea hapa mbona siwaelewi?...

**22. KAREMBO:** Mama, david alinieleza leo shuleni kuwa kuna nyasi aina ya mzumai zinazotumiwa kwa chai na pia hufukuza mbu... nilikuja hapa ilinichukuwe kidogo na tukapande nyumbani kwetu... mimi na david tunahitaji elimu yeyote inayohusiana na maangamizo ya mbu... kwa sababu sisi ndio tunaosimamia chama h cha kupambana na malaria shuleni kwetu..

**23. DAVID:** Na chama hicho kimeorodhesha shule **nzima!**

**24. BETTINA/MAMA DAVID:** (**SURPRISED)** Shule nzima??

**25. KAREMBO:** nimejifunza kuwa kuishinda malaria ni lazima kila mmoja ahusishwe...ni lazima tuwapige vita mbu hawa kwa hali na mali kwa kusambaza elimu na mafunzo kila pahali

**26. MAMA DAVID:** Karembo busara hiyo umeitowa wapi? Una miaka kumi na nne tu lakini unazungumza kwa hekima hata umetufanya sisi watu wazima tusijione maana? Sisi hapa twateteshana tena ilihali wewe na david mumeungana kusema kweli tumewaaibisha sana.

**27. BETTINA: (TONES DOWN HER VOICE)** ) ni kweli watoto wetu...nilikuwa nimekuja kumtaka radhi mamake david kuhusu yale yaliotokea.. na nilitaka anipe ushauri ili na mimi niwe mstari wa mbele katika vita dhidi ya malaria.. lakini tazama yaliozuka...samahani.

**28. MAMA DAVID: (ALSO TONES DOWN VOICE)** ) pia mimi naomba

samahani...

**29. DAVID:** Mama, kwanini basi wewe na mamake karembo musiungane na kuanza kuwafunza wanawake wengine kuhusu matumizi ya nyasi za mzumai katika kufukuza mbu? Nina hakika kuwa wengi wao hawajui faida yake.

**30.KAREMBO:** Ndio! Na kama kuna maua au nyasi nyengine ambazo zinaweza kufukuza mbu pia tunaweza kuzipanda mduara wa nyumba zetu ili kufukuza mbu! Mama, hilo ni wazo zuri!

**31.BETTINA:** Sijui wanangu **(UNSURE)** nafikiri uswahiba wetu hauwezi kurudi kama ulivyokuwa hapo awali....

**32. MAMA DAVID:** Watoto wamesema kweli... najuwa kuna miti na mimea mingi inayofukuza zaidi mbu na wadudu wengineo.

**33. DAVID: (EXCITED)** Kwa hivyo mmekuwa tena marafiki? Munafikiri tunaweza kushinda vita hivi dhidi ya malaria?

**(SHORT SILENCE)**

**34. BETTINA/MAMA DAVID/KAREMBO: (ALOUD)** Ndio tunaweza!!

**(THEY ALL LAUGH)**

**35.BETTINA:** **(REALIZING SUDDENLY)** Tumechelewa sana karembo! Nilimuacha babako peke yake na mtoto lazima awe hivi sasa ameamka kwa njaa....

**36. KAREMBO:** Mama, wacha nichukuwe huo mzumai kidogo kama mamake david atanikubalia halafu twende... sawa?

**37. MAMA DAVID:** usichukuwe kidogo.. chukuwa unaokutosha...

**38. BETTINA:** Basi nitakupitia kesho tupange tutakavyoanza kazi ya kuhamasisha akina mama.. nina mengi yakukueleza...

**39. MAMA DAVID:** nitakusubiri...Mueleze mumeo masika kuwa tumesameheana... na msalimie zawadi... tena umwambie aje aniuzie samaki kama kitambo...

**40. NARRATOR:** Basi betina na karembo walifulizia nyumbani baada ya kuurrudisha uhusiano kati ya familia zao na mamake karembo na mamake david walianza mikakati ya kuhamasisha akina mama wengine kuhusu kujikinga na malaria. karembo na david wakisaidiwa na dkt munga walipata maelezo yote muhimu kuhusu malaria na wakatayarisha michezo, ngoma na mashairi yaliyosomwa na kuigizwa kwa ustadi kwa wanakijiji..baadaye siku ya mtihani ikawadia.

**SCENE THREE: MORNING AT KAREMBO'S SCHOOL ASSEMBLY**

**F-SFX: SCHOOL BELL RINGS.. NOISY VOICES FROM STUDENTS.**

**41. H/TEACHER:** kimya! Kama munavyojuwa mtihani wa kitaifa kwa wananfunzi wetu wa darasa la mwisho unaanza kesho.. nataka kuwe kimya kama maji ya mtungi wakati wote.

**G-SFX: MURMURINGS OF PEOPLE WHO ARE DISSATISFIED**

**42.H/TEACHER:** Kabla hatujaanza masomo ningependa kuwapongeza Karembo na David ambao wamefanya kazi pamoja kwa bidii

**H-SFX: WHISTLES / CHEERINGS FROM STUDENTS**

**43. H/TEACHER:(ANGRY)** kimya! Nilisema hao wawili nawapongeza kwa kufanya bidii wakisaidiana na uongozi wa shule katika hicho chama cha kuangamiza malaria.. nilipata ombi kutoka jopo la elimu la kututaka tuanzishe vyama hivi mashuleni mwetu wilayani Ribo... tuwapigieni makofi...

**I-SFX: HUGE APPLAUSE**

**44. H/TEACHER:** hayo tosha kwa leo... rudini madarasani mwenu... nataka kukutana na viongozi wa chama hicho cha kupambana na malaria...

**J-SFX: NOISES AS STUDENTS DISPERSE FOR CLASS**

**45. H/TEACHER:** karembo na david... nina habari njema kwenu... karembo umealikwa katika kituo cha redio cha humu wilayani katika makala ya ”maisha bora”.. leo jioni kwa hivyo jitayarishe na nakutakia kila la heri katika mtihani wako wa mwisho..

**46.NARRATOR:** Punde si punde kijiji kizima kilijua kuhusu mualiko wa Karembo redioni na jioni ilipowadia wote wakajikusanya ili kusikiliza,Masika alimualika Yakubu nyumbani mwake..

**<u>SCENE FOUR: YAKUBU, BETTINA AND MASIKA AT MASIKA'S HOUSE LISTENING TO RADIO</u>.**

**47. MASIKA:** (**TALKING SOFTLY)** Yakubu,umegunduwa kitu fulani?

**48. YAKUBU:** Ndio,si kumekuwa jioni.

**49. MASIKA:** Simaanishi hivyo... leo kimya kimetanda.. sio kawaida.. (**IMITATES MOSQUITOES)** hawako tena!

**50. YAKUBU:** Eeenhe..sasa nimekuelewa!

**51. BETTINA:** saa zimeshafika... hebu tusikilizeni redio sasa..

**K-SFX: RADIO BEING TUNED**

**52. RADIO PRESENTER:** leo katika studio yetu tunaye kama kawaida dkt Munga kutoka hospitali ya wilaya ya Ribo na pia yupo mgeni wetu mashuhuri atakayetueleza yeye ni nani na amefanya nini katika harakati hizi za kupigana na malaria...

**53. YAKUBU: (CALLS OUT)** Masika! Betina! Kipindi kimeanza! Kimeanza!

**54. MASIKA:** Kimya yakubu! Mbona unapenda sana makelele? Si tuko hapa pamoja!

**55. BETTINA: (CUTS THEM SHORT)** Sasa tutasikiliza redio ama tuizime tuwasikize nyinyi..

**56. RADIO PRESENTER:** Karibu Daktari,hebu anza kwa kutufahamisha malaria ina athari gani katika uchumi wetu?

**57. DR. MUNGA:** Asante, malaria ni ugonjwa unaohusishwa na umaskini, maradhi haya yanatatiza uzalishaji wa jamii katika viwanda na majumbani mwetu na kupunguza mapato katika jamii zilizoathiriwa.

**58. RADIO PRESENTER:** Unataka kusema kwamba matajiri hawaugui malaria?

**59. DR. MUNGA:** Sio hivyo, abadan! Hata wao pia wanauguwa lakini wana nafasi nzuri ya kupambana na maradhi haya... malaria inaweza kutumia hata asilimia 25 ya mapato katika matibabu na kinga yake.. takwimu zinaonyesha kuwa malaria inatumia takriban dola za Merikani bilioni kumi na mbili katika mapato ya jumla ya bara hili..

**60.YAKUBU: (SHOCKED)** Eti dola bilioni kumi na mbili!salaala!na haya mapato ya jumla ndio nini haswa?

**61. MASIKA:** Sssh! Ni njia moja ya kupima hela zilizopatikana na zilizotumiwa..wewe jua tu kuwa tunapoteza senti nyingi.

**62. RADIO PRESENTER:** Hizo ni fedha nyingi mno!je kuna athari nyingine?

**63. DR. MUNGA:** Ndio, malaria pia ni kizuizi kikubwa cha maendeleo katika afrika, waekezaji wa biashara kutoka mabara mengine huhofia kuekeza katika sehemu zinazoathirika na malaria.. na watalii wengi huwa na uoga wa kutembelea maeneo yaliyoathiriwa kwa malaria.

**64. RADIO PRESENTER:** kama ulivyosikia mpenzi msikilizaji.athari za malaria katika uchumi ni kubwa hivyo basi lazima tujitoe muhanga kujikinga. sasa tunamualika mgeni wetu mashuhuri,akiwa na umri wa miaka kumi na nne tu na busara tele ameetoka katika familia zetu za kawaida lakini kwa ajili ya juhudi zake viwango vya malaria vimeshuka kwa miezi tu! Karibu kituoni karembo!

**65. KAREMBO: (SHY AND SOFTLY)** Asante..

**66. MASIKA/BETTINA: (PROUDLY CHEERING)** Binti yetu..yeeee!

**67. YAKUBU: (SARCASTIC)** Sasa ni nani mwenye kelele?

**68. RADIO PRESENTER:** kabla ya kuendelea na karembo, kwanza tupate muziki kidogo alafu tutarudi papa hapa tupate nasaha ya mgeni wetu ambaye amefanya kazi kubwa ya kuiangamiza malaria... usiondoke msikilizaji.

**MUSIC INTERLUDE**

**OUTRO/NARRATOR:**

Basi karembo akawahadithia tena wasikilizaji kuhusu mkasa wake huku akiwatoa machozi wazazi wake na kuamsha nguvu mpya za kupambana na malaria kwa wasikilizaji wote wa kipindi. kwa sababu yake na wengineo waliojitolea , mbu waliadimika katika wilaya hiyo.Ilikuwa ni sememu ya mwisho ya mchezo "**WAGENI VIZABIZABINA-VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA''**.Ni matumaini yetu ulifurahia na kuelimika . Usisahau kuwa unapotaka kusikiliza tena au kutupa maoni yako tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe